SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.21 NO. 2 2022
DOI: 10.51984/JOHS.V21I2.1902

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Vionjo Vya Fasihi Simulizi Katika Riwaya Ya "Dar Es Saalam Usiku"

Saad Buoazuom Mehemed

African Languages, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Wanawake
Mazingira
Riwaya
Tabia
Mbalimbali
Makala
Malengu

**ABSTRACT**

Makala haya inachunguza vionjo vya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika riwaya ya Kiswahili. Riwaya iliyochambuliwa katika makala haya ni "Dar es Salaam Usiku", iliyoandikwa na Ben R. Mtobwa. Kwa kuwa makala haya yanachunguza vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya (ambayo ni utanzu wa fasihi andishi), nadharia ya mwingilianomatini au mwingilianotanzu ilitumika katika kukusanya na kuchambua data.

katika makala haya tulipata jibu kwa maswali yalilosema Je; Tanzu mbalimbali za fasihi zinaweza kusimama kivyake pasipo kuingiliana? Je; mwandishi anaweza kuunda mseto wa tanzu mbalimbali katika kazi yake kwa kuzichanganya ili kuunda kazi moja. Na kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya kunaborsha zaidi uwasilishaji wa ujumbe?.

## إلهام الأدب الأصلي: أمثلة من رواية ليلة دار السلام

سعد ابوعزوم امحمد علي

اللغات الإفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
المرأة
طبيعة
الادب
العادات
مختلفة
المقالة
الرواية
نظرية
الاهداف

**الملخص**

في هذه المقالة نستكشف الأنواع الفرعية المختلفة للأدب الشفوي من خلال الرواية السواحيلية التي تم تحليلها في هذا المقال وهي رواية " دار السلام ليلا" بقلم بن متوبوا. نظرًا لأن هذه المقالة تبحث في وجهات نظر الأدب الشفوي في الرواية (وهو نوع مختلف من الأدب المكتوب) ، فقد تم استخدام نظرية التفاعل المتشابك أو التفاعلي في جمع البيانات وتحليلها.

وفي هذه المقالة أيضا إجابة على الاسئلة التالية: هل يمكن لأنواع الأدب المختلفة أن تأتي بمفردها دون أن تتفاعل مع غيرها؟ هل يمكن للكاتب إنشاء مجموعة من الأنواع المختلفة في عمله من خلال الجمع بينها لإنشاء عمل واحد ( هجين). وهل سيؤدي وجود نكهات الأدب الشفهي في الرواية إلى زيادة تحسين إيصال الرسالة الأدبية؟.

## UTANGULIZI

*Fasihi simulizi na fasihi andishi ni aina mbili za fasihi ambazo, licha ya kuwepo kwa sifa nyingi zinazozitofautisha, hutofautiana kwa kiasi kikubwa katika njia ya uwasilishwaji. Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo h uku fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi. Fasihi simulizi imegawanyika katika tanzu mbalimbali ikiwemo semi, nahau, methali, vitendawili, ngomezi, hadithi, ngoma, majigambo, nyimbo/mashairi, na tanzu zinginezo. Kwa upande mwingine, fasihi andishi yenyewe imegawanyika katika tanzu za ushairi, tamthiliya na riwaya. Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza vionjo vya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika riwaya. Riwaya iliyochambuliwa katika makala haya ni Dar es Salaam Usiku iliyoandikwa na Ben R. Mtobwa. Kwa kuwa makala haya yanachunguza vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya (ambayo ni utanzu wa fasihi andishi), nadharia ya mwingilianomatini au mwingilianotanzu ilitumika katika kukusanya na kuchambua data.*

## NADHARIA YA MUINGILIANOMATINI

Wamitila (2002), Njogu na Wafula (2007) na Ndumbaro (2013), wanafafanua Mwingilianomatini kama moja ya nadharia za fasihi, ambayo hutumika katika

*Corresponding author:
E-mail addresses: saa.ali@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 26 May 2022 - Received in revised form 14 August 2022 - Accepted 30 August 2022*

kuchunguza, kuchambua data na kubaini uwepo wa kazi moja ndani ya kazi nyingine katika kazi za fasihi. Nadharia hii iliasisiwa na, Julia Kristeva, raia wa Ufaransa ambae alizaliwa mwaka 1941 nchini Bulgaria. Kristeva aliasisi nadharia hii ya Mwingilianomatini kufuatia uchunguzi alioufanya juu ya nadharia ya Usemezano ya Mrusi Mikhail Bakhtin (1895 – 1975). Kwa mujibu wa Bakhtin, nadharia ya Usemezano huamini kuwa kazi ya fasihi ina alama ya sauti ambazo huingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia hapo awali, zilizopo, au zijazo. Kwa mantiki nyingine tunaweza kusema kwamba kazi moja inaweza kuacha athari au alama zake katika kazi nyingine za sasa ama za badae. Kupitia nadharia hii, Kristeva aliweza kuendeleza mawazo haya ya nadharia ya usemezano na akaibuka na nadharia yake ya mwingilianomatini ilipotimu mwaka 1960. Katika nadharia ya mwingilianomatini, Kristeva anaamini kuwa hakuna kazi inayojitegemea bali kazi zote hutokana na msingi wa kazi zingine ambazo huungana na kuunda kazi moja ambayo inaweza kutumika katika miktadha mbalimbali. Kwa tafsiri nyingine, kazi za fasihi ni matokeo ya mchangamano wa kazi mbalimbali za fasihi ambazo zimetangulia kwani mwandishi hupata mawazo kutoka katika kazi mbalimbali kabla hajaandika. Nadharia ya mwingilianomatini inaongozwa na msimamo wa kwamba matini hufanana na kuchangizana, hivyo matini ya kifasihi haiwezi kujitegemea peke yake pasipo kupata athari za namna yoyote kutoka kwenye kazi zingine zilizoitangulia. Saleh (2015) anadai kwamba nadharia ya mwingilianomatini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ile tajriba ya uingiliano wa mitindo ya kitaashira na kwamba nadharia ya mwingilianomatini ni jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya kazi kuwa na maana kamili, ambapo dhana ya matini huangaliwa kama ina utegemezi na matini nyengine kwa kuitwa "mwanda wa ki – mwingilianomatini". Saleh, (2015) anaenda mbali zaidi kwa kusema kwamba matini yoyote ile huchukua au kujipamba kutokana na kazi nyingine kwa kuzichawanya katika mawanda ya kimwingilianomatini.

Kwakuwa makala haya yanachunguza vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya, nadharia iliyofaa zaidi ni nadharia ya Mwingilianomatini. Katika makala haya, nadharia ya mwingilianomatini imetumika ili kuchunguza na kubainisha matumizi ya mbinu ya fasihi simulizi katika riwaya teule ya Dar es salaam Usiku, iliyoandikwa na Ben Mtobwa. Kwa kutumia nadharia hii, makala haya yameweza kuonyesha uhusiano na kuathiriana kwa kazi za fasihi simulizi katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku iliyoandikwa na Ben Mtobwa. Katika makala haya, nadharia ya mwingilianomatini imesaidia sana katika kubainisha vipengele vya fasihi simulizi kama vile; nyimbo/ushairi, ufutuhi au matani, methali, semi, nahau, majigambo, na vingine. Nadharia hii pia imesaidia katika kubaini na kufafanua dhamira zilizojitokeza kutokana na kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya teule ndani ya makala haya. Hivyo, nadharia ya mwingilianomatini ilitumika kuchunguza na kubaini vionjo vya fasihi simulizi vilivyopo katika fasihi andishi kwa kutumia riwaya ya Ben Mtobwa inayoitwa Dar es Salaam Usiku.

## DHANA YA MWINGILIANOMATINI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

Dhana ya mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili, imejadiliwa na wataalam mbalimbali, miongoni mwao ni Wamitila (2002), Wamitila (2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Adam (2014). Wamitila (2008) anaiona dhana ya mwingilianomatini kama kuhusiana na kutegemeana kwa matini au kazi za kifasihi na matini au kazi za kifasihi zilizotangulia. Wamitila anasisitiza kwamba uhusiano huu unaweza kujumuisha vipengele vya fani na maudhui katika fasihi. Senkoro (2011) anafafanua dhana au mbinu ya mwingilianomatini katika fasihi kama kutumika kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kuwasilisha maudhui ya kazi ya fasihi iliyopo kwenye utanzu mwingine: mfano, kutokea kwa nyimbo ndani ya ngano au simulizi ni mwingilianomatini kwa mantiki ya kwamba wimbo unatumika katika simulizi au ngano kubeba maudhui fulani. Senkoro anaenda mbali zaidi na kudai kuwa mwingilianomatini ni kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi Fulani ya fasihi.

Kwa upande wake Herman (2011), mwingilianomatini ni mtindo wa kuchanganya vipengele mbalimbali vya kisanaa katika kazi moja ya fasihi. Katika kutoa ufafanuzi, Herman anadai kuwa, mwandishi wa kazi ya fasihi hujikuta amechanganya matini za nyimbo, semi, hadithi, hadithi ndani ya hadithi, maigizo na matumizi ya ishara katika kazi yake ya fasihi. Mtindo huo wa kuchanganya vipengele tofauti katika kazi moja ya fasihi ni kitu kilichozoeleka sana miongoni mwa wanafasihi.

## VIONJO VYA FASIHI SIMULIZI KATIKA RIWAYA YA DAR ES SALAAM USIKU

Makala haya yamebaini kuwa mwandishi ametumia tanzu tofauti tofauti za fasihi simulizi katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku ili kuibua dhamira au maudhui ndani ya kazi yake. Zifuatazo ni tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zilizotumika kama kionjo cha ufasihi simulizi katika riwaya.

### MATUMIZI YA USHAIRI/NYIMBO

Shairi linafafanuliwa na Mulokozi (1996) kama utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno wenye kusawiri hisia, wazo, hali, kitu au tukio fulani na papo hapo kuvuta au kuathiri hisia zetu badala ya kutumia lugha nathari. Makala haya yamebaini matumizi ya ushairi katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku ambapo mwandishi ametumia ushairi kama matini yanayoweza kuibua au kubeba ujumbe katika riwaya yake. Matumizi ya ushairi ndani ya riwaya ni ushahidi dhahiri wa kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi. Tazama mfano ufuatao:

*Ndiyo…furaha tele moyoni*

*Kwani sura ya huyu mwandani,*

*Ni kama nuru ya mwezi,*

*Na ngozi yake laini,*

*Kama maji matamu jangwani.* (Uk. 30)

Mtunzi ametumia ushairi ama nyimbo (ambazo ni tanzu ya fasihi simulizi). Kwa kuingiza ufasihi simulizi katika riwaya yake, mwandishi anaibua jumbe mbalimbali na kuboresha zaidi maudhui ya kazi yake. Nyimbo hizi alizotumia mwandishi katika riwaya yake zinaibua sana dhamira ya mapenzi hivyo, anafanikiwa kuonesha hisia walizobeba wahusika, mathalani Rukia na Peterson ambao wanaelezwa kuwa katika penzi zito.

### MATUMIZI YA SEMI

Wataalamu wengi wamefafanua maana ya semi. Finegan (1979), Mulokozi (1996:35), na Wamitila (2003:135) wote wanaafiki ya kuwa semi ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi. Katika kufasili semi, wataalamu hawa wanaafiki kuwa semi ni kauli au tungo fupifupi zinazobeba misemo pamoja na mafumbo yanayopelekea kupatikana kwa mafunzo katika jamii". Mifano ifuatayo inaonyesha matumizi ya semi katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku iliyoandikwa na Ben R. Mtobwa.

*Alikuwa amekusudia* ***kumchezesha kindumbwendumbwe*** *hadi bwana huyu na mapesa yake, na masuti yake, ajione hamnazo kama si hayawani katika halaiki.* (Uk. 31)

Kumchezesha mtu ***kindumbwendumbwe*** humaanisha kumuadhibu mtu kwa kumuhangaisha mbele ya halaiki. Matumizi ya msemo huu katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku yamechangia katika kuibua dhamira ya mapenzi ya uongo au mapenzi yasiyo ya dhati kwani ni dhahiri kabisa kuwa Rukia alikuwa na lengo la kumdharirisha Peterson kwa kumuinua acheze muziki mbele ya watu wengi. Kwakuwa semi ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi, ujitokezaji wake katika riwaya unadhihirisha wazi kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi.

*Kula vizuri, kulala vizuri, kuvaa vizuri, kupanda magari mazuri,kusoma n.k. usingeishi kwa kulala vichochoroni na kuokota chakula* ***kama mbwa koko*** (Uk. 4)

'Mbwa koko' ni msemo katika lugha ya Kiswahili ambao humaanisha mbwa asiyetunzwa na mfugaji na hujipatia chakula kwa kuzurura mtaani. Katika riwaya hii, msemo huu umetumika kuibua dhamira ya umaskini au ufukara unaowakabili Hasira, Hasara, na watoto wengine wanaoishi mitaani. Hii ni dhahiri kwamba katika riwaya hii, mwandishi ametumia vionjo vya fasihi simulizi katika fasihi andishi ili kujenga zaidi maudhui ya kazi yake.

*Sasa Hasara alikuwa* ***riwaya ya kusisimua*** *katika mtaa wa Manda na vichochoro vyake.* (Uk. 130)

Msemo 'riwaya ya kusisimua' umetumika kusisitiza namna Hasara alivyobadilika na kujikuta akipendwa na wanawake wengi tofauti na alivyokuwa hapo awali. Hivyo msemo huu haujatumika tu pasipo na sababu yoyote bali ni mbinu sahihi ya muingilianotanzu aliyoichagua mwandishi katika kujenga kazi yake.

*Waliwapeleka katika majaa madogo madogo ambayo walijipatia mabaki ya chakula na matunda, na yale majaa ya* ***uzunguni*** *ambako waliokota vitu vizuri vizuri na kuviuza mitaani.* (Uk. 103)

Katika kusawiri dhamira ya kuwepo kwa matabaka katika jamii, Ben Mtobwa

ametumia msemo **'uzunguni'** ambao katika lugha ya Kiswahili humaanisha mitaa inayokaliwa na watu wenye kipato cha juu ukilinganisha na wale wenye kipato duni ambao ndiyo wanawakilishwa na wahusika wengi katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku. Msemo huu unadhihirisha wazi kabisa kwamba utanzu mwingine wa fasihi unaweza kutumika katika utanzu mwingine ili kuleta ladha au kuibua zaidi maudhui.

**MATUMIZI YA NAHAU**

Nahau zinafasiliwa na wataalamu wengi kama kauli fupi fupi zinazotumia sana lugha ya picha. (R. Kaduguda , J . Kiango na T. Ipara 2015) maneno yanayotumika katika nahau yanaweza kuwa maneno ya kawaida lakini maana yake huwa tofauti kabisa na maana za kikamusi za maneno yanayounda nahau. Ili kupata maana halisi ya nahau, inashauriwa kuangalia maana ya ndani kabisa ambayo inakuwa imeshatengenezwa na watumiaji wa lugha husika na sio kuangalia maana za maneno yanayounda nahau. Juma (2016) anadai kuwa aghalabu nahau huundwa kwa kitenzi na nomino. Tazama mifano ifuatayo:

*Mara moja wakawa kama **chanda na pete** katika mchezo. Hatua zao **zilioana**, miondoko yao ilirandana* (Uk. 32)

***Aliitupia jicho** jingine saa yake……..*(Uk. 42)

*Mawazo! "Sina mawazo yoyote" Alimjibu **akiiba jicho** na kutazama tena saa yake.* (Uk.17)

Nahau **'tupia jicho'** au **'kuiba jicho'** katika lugha ya Kiswahili humaanisha kuangalia kitu fulani kwa haraka. Nahau hizi hutumika kila siku katika mazungumzo baina ya watu. Vile vile , mwandishi ametumia nahau ***chanda na pete*** ambayo humaanisha hali ya kuwa marafiki ili kutia msisitizo juu ya namna urafiki baina ya Rukia na Hasira ulivyoanza hadi kufikia hatua ya kuwa wapenzi hapo badae. Matumizi ya nahau huipa ladha ya kisanii kazi ya fasihi na kuifanya yenye kuvutia kimuundo na hata kimaudhui. Vilevile, neno ***zilioana*** katika mfano hapo juu ni nahau inayomaanisha kurandana, kufanana au kuendana. Utokeaji wa nahau, ambazo ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi, katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku unadhihirisha kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi katika fasihi andishi.

**MATUMIZI YA METHALI**

Methali ni dhana ambayo imefasiliwa na wataalamu lukuki wa lugha ya Kiswahili. Mulokozi (1996) kama alivyonukuliwa na Juma, (2016), ana maoni kwamba, "methali ni usemi mfupi wa mapokeo unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na tajriba (uzoefu wa maisha) ya jamii inayohusika". Kwa upande wake Senkoro (1984), methali ni sehemu ya lugha ambayo inaweza kufananishwa na kiungo cha lugha na kitoweo cha lugha na pia methali hutumiwa kwa kuyatafakari na kuyapima maisha, kufunzia jumuiya na kutawalia jamii na mazingira ya binadamu. Anaongeza kwamba, methali hufichua zaidi dhamira zinazobebwa na utamaduni wa jamii fulani pamoja na hekima na busara za watu wanaotumia methali katika mazungumzo. Tazama mfano ufuatao

*Au ndio yale yale ya mbuzi wa maskini, ambayo yanaanza kumtokea?* (Uk. 125)

Katika mfano huo hapo juu, mwandishi ametumia methali *'mbuzi wa maskini'* ambayo siku zote hukamilishwa na kishazi *'hazai'*. Methali hii imetumika kusisitiza kwamba ni vigumu sana masikini kufanikiwa kama ilivyo kwa Hasara, muhusika alietokea katika familia isiyo na kipato chochote. Methali ni utanzu wa fasihi simulizi na utokeaji wake katika riwaya ambayo ni utanzu wa fasihi andishi unathibitisha hoja ya kwamba utanzu mmoja unaweza kutumika katika ujenzi wa kazi nyingine ya fasihi ambayo ipo kwenye utanzu tofauti kabisa.

**MAZUNGUMZO**

Mazungumzo baina ya wahusika katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku yameundwa katika namna mbalimbali. Makala haya yamebaini muundo wa ufutuhi, marumbano na hotuba katika riwaya hii. Ufutuhi na marumbano ni vionjo vinavyojitokeza sana katika fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Ponera (2010 na 2014), ufutuhi ni mjumuiko wa hali za uchangamfu, furaha na kicheko inayotokana na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto. Kwa kawaida, maneno, matendo, au matukio hayo yenye uwezo wa kuzua hali hiyo ya ufutuhi huwasilishwa kwa kutumia vipengele mbalimbali vya kisanaa kama vile kejeli, dhihaka, ufyosi, ubeuzi, tashtiti na utani. Katika riwaya ya *Dar es Salaam Usiku*, mwandishi ametumia miundo mbalimbali ya mazungumzo ili kuleta vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya yake. Tazama mfano ufuatao, ambao msimuliaji katika riwaya hii anadai kuwa hii ilikuwa hotuba ya Hasira kwa rafiki yake Hasara juu ya umuhimu wa kupambana kwaajili ya kupata maisha bora.

***Hotuba***

*"Machozi ya mwanaume hayana thamani yoyote. Ni machozi ya mwanamke tu ambayo yanaweza kumsaidia. Una bahati mbaya kuzaliwa mwanaume na huwezi kujibadili. Iliyobaki ni kupambana. Vumilia kwa kula haya matakataka, pata afya kwa huu uchafu, ukue. Ukipata umri wa kutosha, fanya juu chini uondokane na mateso haya. Kuna njia nyingi za kujikomboa. Zote zinahitaji moyo na mapambano. Fanya kila njia, na kila kitu ili ujikomboe." Ilikuwa hotuba fupi, lakini yenye uzito wake.*

Matumizi ya hotuba yanadhihirisha kuwa mwandishi ametumia vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya yake ili kutia mkazo katika dhamira ambazo zinaibuliwa ndani ya riwaya kutokana na mazungumzo ya wahusika.

***Ufutuhi***

*"Wewe….unadhani tutakwita 'wewe' hadi lini?…. Tuambie jina lako"*

*"jina"! Aliduwaa.*

*"Ndiyo… kila mtu ana jina"*

*"Mie sina…"*

*"Lazima uwe na jina. Tafuta jina"*

*"Sina"*

*"Basi tutakuita Hasara"*

*"Hasara!"*

*"Ndiyo. Tangu leo wewe Hasara. Sawa?*

Katika mfano huu, mwandishi ametumia lugha ya utani kwa kuonesha namna Hasira na wenzake wanavyompatia jina Hasara kupitia lugha ya utani na jina linakuwa lake katika maisha yake yote. Mbinu hii ya utani inatokana na mazungumzo ya kawaida ambamo watu hutaniana na pengine kupeana vijembe. Vionjo hivi katika fasihi andishi vimesaidia kuibua dhamira ya umaskini katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku kwani tunaona kwasababu ya umskini, Hasara anakubali kupewa jina linalosadifu uhalisia wa maisha yake pasipo kupinga chochote.

**MATUMIZI YA MAJIGAMBO**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) kama alivyonukuliwa na Mningo, (2015) majigambo ni aina ya maghani au sifo yanayohusu kujisifu au sifa, aghlabu kuhusu kutongoa utungo wa kujisifu kuhusiana na kitendo fulani cha ushujaa, urijali au matendo muhimu. Kufuatia upembuzi katika riwaya ya Dar es Salaam Usiku, makala haya yamebaini matumizi ya majigambo katika matini hiyo. Kwa kuwa majigambo ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi, ujitokezaji wake katika riwaya hii ya Dar es Salaam Usiku unadhihirisha kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Tazama mfano ufuatao.

*Awe na jeuri…awe na kasoro… hapa ametu," Rukia alinong'ona. Nitamwonyesha kuwa Rukia siyo mtu wa kurukia hovyo. Jasho litamtoka. Asipojihadhari, hata chupi ataiuza… awe waziri, awe balozi…*(Uk. 2)

Katika mfano huu, tunaona Rukia anatumia majigambo kueleza uzuri wake na namna ambavyo anaweza kumshika mwanaume yeyote na kumuadhibu kimahaba anavyotaka yeye. Mwandishi ametumia majigambo ambayo ni matini ya fasihi simulizi ili kujenga zaidi maudhui katika riwaya yake kwa kuonesha zaidi jeuri ambayo Rukia anayo kutokana na uzuri alionao. Vionjo hivi vya fasihi simulizi katika riwaya vinaonesha kuwa mwandishi anaweza kutumia utanzu tofauti wa fasihi katika kazi yake ili kuibua zaidi maudhui.

**HITIMISHO**

Makala haya yameshughulikia kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya. Baada ya mapitio ya maandiko mbalimbali, makala haya yamegundua

kuwa tanzu mbalimbali za fasihi zinaweza kusimama kivyake pasipo kuingiliana lakini pia kwa sababu za kitaalamu kwa malengo ya kisanii zaidi, mwandishi anaweza kuunda mseto wa tanzu mbalimbali katika kazi yake kwa kuzichanganya ili kuunda kazi moja. Hivyo basi, kuwepo kwa vionjo vya fasihi simulizi katika riwaya kunaborsha zaidi uwasilishaji wa ujumbe.

**MAREJELEO**


Finnegan, R. (1979). *Oral literature in Africa*. Nairobi, Oxford University Press.

Herman, L (2011) "*Dhana ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili"* Makala katika Kioo cha Lugha: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Juma, N. H. (2016). "*Kuchunguza Fani Na Dhamira Katika Semi Zilizoandikwa Katika Vyombo Vya Safari Vya Baharini Kisiwani Pemba*." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kaduguda, R., Kiango, J & Ipara, T. (2015). *Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha kwanza*

Mningo, A. R. (2015). "*Tathmini Ya Mwingilianomatini Katika Utunzi Wa Emmanuel Mbogo*: Utafiti Linganishi Wa Tamthiliya Ya Ngoma Ya Ng'wanamalundi Na Fumo Liongo"

Mulokozi, M.M (1996), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam.

Ndumbaro, E (2013) *"Taathira katika Fasihi: Msingi wa kuwepo motifu za aina moja katika Tanzu anuai za Fasihi za mataifa /makabila tofautitofauti ulimwenguni*" makala katika chombez.blogspot.de/2013/10/taathira-katikafasihi.html?m=1 Bubujiko la Maarifa, Jumapili, tarehe 13 Machi.

Njogu K & Wafura, (2007) *Nadharia za uhakiki wa fasihi*, Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.

Ponera, A.S. (2010). "*Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert*: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa, na Athari Zake kwa Wasomaji." Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma. Ponera, A.S. (2014). "Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban.

Ponera, A.S. (2014). "*Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili*: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban.

Wamitila, K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi*: Misingi na Vipengele vyake, Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

Wamitila, K.W (2003) *Kamusi Fasihi*: Istalahi na Nadharia, Focus Publication Ltd, Nairobi, Kenya.